CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI

HOTUBA YA MAKAMU MKUU WA CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI – MUHIMBILI; PROFESA EPHATA KAAYA KWENYE MAHAFALI YA SABA YA MUHAS

TAREHE 14 DESEMBA 2013

Mkuu wa Chuo, Mheshimiwa Rais Mstaafu Alhaji Dkt. Ali Hassan Mwinyi,

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb),

Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dk Hussein Mwinyi (Mb),

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Mhe. Deogratias Aloys Ntukamazina (Mb),

Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili,

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Dkt. Marina Njelekela,

Waheshimiwa Mabalozi,

Viongozi Waandamizi wa Serikali,

Maprofesa na Wahadhiri,

Wazazi na Walezi,

Wahitimu,

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Kwa niaba ya Wanajumuia wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, ninayo heshima kubwa kukukaribisha Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, kwenye mahafali haya ya saba tangu Chuo hiki kiwe Chuo Kikuu kamili. Napenda pia kukushukuru kwa kukubali kuja kuwatunukia stashahada na shahada mbalimbali wahitimu wetu wa leo.

Aidha napenda pia kuwakaribisha na kuwashukuru wageni waalikwa, viongozi wa Serikali, viongozi wa taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali, mabalozi, wazazi, walezi, ndugu na marafiki kwa kukubali mwaliko wa kushiriki nasi katika sherehe hii ya mahafali. Karibuni sana.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wahitimu wote wa leo kwa kufaulu vizuri masomo yao licha ya changamoto mbalimbali za kitaaluma na kijamii katika kipindi cha masomo yao. Ni imani yangu kwamba mtakuwa mabalozi wazuri wa Chuo hiki chenye sifa nzuri kitaifa na kimataifa kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa na kuzingatia miiko ya taaluma zenu.

Mafanikio yaliyofikiwa leo na wahitimu hawa yasingeweza kupatikana bila ya mchango mkubwa wa Serikali, Maprofesa, Wahadhiri, wafanyakazi wengine wa Chuo, wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, wa Taasisi nyingine za afya walizojifunzia, wazazi, ndugu, jamaa na marafiki ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia kuwawekea mazingira mazuri ya kuhitimu masomo yao leo. Hawa wote pia wanastahili shukrani zetu na pongezi nyingi.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe Mkuu wa Chuo, na kwa Baraza la Chuo likiongozwa na Mheshimiwa Deogratias Ntukumazina kwa kuendelea kuwa karibu sana na

Chuo na kukisaidia mapema pale changamoto zinapotokea, mpaka tukaweza kufanikiwa na kufika hapa tulipo.

Aidha naomba niungane na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, na kwa niaba ya Jumuiya ya wanachuo wote, kukupongeza kwa kuteuliwa tena na Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili uendelee kuwa Mkuu wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kwa kipindi kingine cha miaka sita (6). Hii inatokana na uwezo wako wa hali ya juu uliouonyesha katika kukisimamia na kukiendeleza Chuo toka kianzishwe mwaka 2007. Tunakuhakikishia kuwa tutaendelea kufanya kazi nawe kwa karibu sana ili Chuo kiweze kupata mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Baada ya kusema hayo, napenda kuchukua fursa hii kuwatambulisha kwako wahitimu wa mahafali ya leo ambao muda mfupi ujao utawatunukia stashahada na shahada mbalimbali za Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili. Katika mahafali haya tuna jumla ya wahitimu **733,** kati yao wahitimu **277** watatunukiwa stashahada na wahitimu **8** watatunukiwa stashahada za juu katika fani mbalimbali za sayansi shirikishi za afya. Pia wahitimu **262** watatunukiwa shahada ya kwanza na wahitimu **186** shahada ya uzamili.

Aidha kati ya wahitimu hawa wa uzamili wahitimu **16** ni wa kwanza kuhitimu kutoka katika programu tatu mpya. Wahitimu **8** ni wa programu ya Huduma ya Dharura, yaani *Emergency Medicine,* **7** ni wa programu ya Tiba ya Saratani, yaani *Clinical Oncology* na **mmoja** ni wa programu ya Urolojia, yaani *Urology*.

Kwa mwaka huu asilimia **36.8** ya wahitimu wote ni wanawake. Azma ya Chuo ni kuwa na asilimia sawa kati ya wahitimu wa kike na wa kiume. Hata hivyo ingawa Chuo kinaendeleza mpango wake wa kuhamasisha wanafunzi wa kike kujiunga na kozi mbalimbali, kwa miaka kadhaa sasa Chuo hakijawa na ongezeko la kuridhisha kwa wahitimu wa kike. Tatizo ni kukosekana kwa

wanafunzi wa kutosha wa jinsia ya kike wenye sifa zinazotakiwa kuja kusomea programu mbalimbali hapa Chuoni. Ili tufanikiwe katika azma hii ni lazima jamii, Serikali na wadau mbalimbali wa elimu, tukiongozwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kubuni na kutekeleza mikakati ya makusudi ya kuwawezesha wasichana kusoma masomo ya sayansi ili wakimaliza masomo ya kidato cha sita na wakiwa na sifa zinazohitajika waweze kujiunga na kusomea programu mbalimbali zinazotolewa hapa MUHAS.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Chuo kinatambua umuhimu na uharaka wa kupata wataalamu wengi katika sekta ya afya nchini. Ili kuhakikisha kwamba miundombinu tuliyonayo inatumika kikamilifu katika upatikanaji wa wataalamu hawa kwa wingi, Chuo kimeanzisha programu tano za stashahada ambazo zinaendeshwa jioni (*evening programmes*) ambazo ni stashahada ya Ufamasia, stashahada ya Uuguzi, stashahada ya Ufundi Maabara, na stashahada ya Afya ya Mazingira na stashahada ya Radiografia ya Uchunguzi wa Magonjwa. Vile vile kwa mwaka huu, Chuo kimeanzisha programu mpya ya shahada ya kwanza Sayansi ya Maabara ya Tiba yaani *Bachelor of Medical Laboratory Sciences (General)*. Hii inafanya Chuo kuwa na jumla ya programu 14 za shahada ya kwanza.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Kulingana na Mpango Mkakati wa Chuo wa miaka mitano (2009/2010 – 2013/2014), kwa mwaka huu Chuo kimetekeleza malengo na majukumu yake kupitia Skuli, Kurugenzi na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

1. **Skuli ya Tiba**

Katika kutekeleza mitaala inayosisitiza yale ambayo mwanafunzi anafanya atakapohitimu (*competence based curricula*), kwa

mwaka huu wanafunzi wa udaktari wa mwaka wa tatu wameanza mafunzo ya vitendo mapema zaidi. Hii itamuwezesha mwanafunzi kupata ujuzi zaidi wa vitendo katika fani hii ya udaktari. Hata hivyo utekelezaji wake unasababisha msongamano zaidi wa wanafunzi katika Hospitali ya Taifa, Muhimbili. Kwa kutambua hilo, Chuo kupitia Skuli yake ya Tiba kipo katika hatua za mwisho za kuingia mkataba wa makubaliano na hospitali ya wilaya ya Bagamoyo ili nayo pia itumike kwa mafunzo hayo.

Aidha katika kupanua wigo wa shughuli za kuongeza pato la ndani, Chuo kupitia Skuli ya Tiba na skuli nyingine, kinaandaa mkakati wa kutumia eneo lake lililoko barabara ya Uporoto kujenga jengo litakalotumika kama hospitali yenye kutoa huduma maalumu za uchunguzi na tiba katika fani mbalimbali za afya. Licha ya kutumika kama chanzo cha mapato ya ndani, hospitali hii itapanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya katika jiji la Dar es Salaam.

2. Skuli ya Afya ya Kinywa na Meno

Ili kuboresha huduma na ufundishaji, Chuo kwa kupitia Skuli ya Afya ya Kinywa na Meno kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali lenye makao makuu yake New York, Marekani linaloitwa *Miracle Corners of the World* kimeanza mchakato wa kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa kukusanya na kutunza taarifa za wagonjwa wa afya ya kinywa na meno. Vile vile katika mradi huu, Chuo kitabadilisha mfumo wa x-ray uliopo sasa ambao ni wa kizamani kuwa wa kidigitali ili kuboresha uchunguzi wa magonjwa ya kinywa na meno.

Kipekee kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi yake binafsi ya kufanya mazungumzo na wafadhili hawa na kuwashawishi ili waendelee kukisaidia Chuo katika kuboresha vifaa vya kufundishia na kutolea huduma katika Skuli ya Afya ya Kinywa na Meno.

3. Skuli ya Famasia

Chuo kwa kupitia maabara yake ya utafiti na maendeleo (*Research and Development*) iliyoko chini ya Skuli ya Famasia kimeingia mkataba na shirika la Marekani linaloitwa *Management Sciences for Health (MSH)* kwa ajili ya kuboresha huduma ya kuhakiki ubora wa madawa hapa nchini. Mkataba huo pia unajumuisha ukarabati wa maabara moja zaidi. Ukarabati huo umeshaanza na tunatarajia utakamilika mwanzoni mwa mwezi Januari 2014. Baada ya ukarabati huu kukamilika tunatarajia kwamba, Skuli ya Famasia itakuwa na uwezo mkubwa na ubora wa hali ya juu miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki katika uhakiki wa ubora wa madawa.

Vile vile, Katika mwaka huu walimu wa skuli ya Famasia walipata mafunzo endelevu katika somo la usimamizi na usambazaji wa madawa *(Supply Chain Managemement)* yaliyoendeshwa na shirika la kimarekani linaloitwa *John Snow Inc (JSI-USAID).* Mafunzo haya kwa walimu yamesaidia sana kuboresha ufundishaji wa somo hili kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza na ya pili katika fani ya Famasia.

4. Skuli ya Uuguzi

Kutokana na upungufu wa walimu katika vyuo vyote vya uuguzi na ukunga vinavyokaribia 80 nchini Tanzania, Chuo kwa kupitia Skuli yake ya Uuguzi kimeandaa programu ya kufundisha walimu wa uuguzi na ukunga katika ngazi ya shahada ya kwanza yaani *Bachellor of Science in Nursing Education*. Programu hii imekamilika na iko katika hatua za mwisho za kupitishwa tayari kwa kuanza kutumika mwakani. Tunaamini kuwa kwa kufundisha walimu wengi katika fani hii, Chuo kitatoa mchango mkubwa katika kupunguza vifo vya kina mama na watoto na kuboresha huduma za afya nchini.

5. Skuli ya Afya ya Jamii

Katika kutekeleza malengo ya Mpango Mkakati wetu Chuo kimeendelea kuongeza programu mpya za uzamili ambazo wahitimu wake wanahitajika sana katika soko la ajira. Katika mwaka huu wa masomo wa 2013/2014 Chuo kwa kupitia Skuli yake ya Afya ya Jamii kimeanzisha programu mpya ya uzamili ya Sayansi ya Afya Kazini na Mazingira, yaani *Master of Science in Environmental and Occupational Health.* Vile vile Skuli imeandaa mtaala wa programu ya uzamili ya Usimamizi wa Biashara katika sekta ya Afya, yaani *Master of Business Administration – Health* ambayo itaanza rasmi mwaka ujao wa masomo.

Aidha katika jitihada za kwenda sambamba na ukuaji wa TEHAMA ulimwenguni hasa hasa katika mafunzo, Chuo kwa kupitia Skuli yake ya Afya ya Jamii kinatarajia kuanzisha programu ya shahada ya uzamili ya Afya ya Jamii (*Master of Public Health*) kwa kutumia mafunzo ya mbali, yaani *Distance Learning*. Mtaala wa programu hii uko katika hatua za mwisho za kupitishwa na utaanza rasmi mwezi Oktoba mwakani.

6. Kurugenzi ya Huduma za Maktaba

Chuo kupitia Kurugenzi yake ya Maktaba kimeendelea kuboresha utoaji wa huduma za vitabu na majarida ya machapisho mbalimbali yaliyoko katika mfumo wa kieletroniki, kwa watumiaji wa Maktaba wakiwemo walimu, wanafunzi na watafiti mbalimbali kutoka ndani na nje ya Chuo. Chuo kinatoa shukrani za dhati kwa wafadhili walioendelea kuwezesha upatikanaji wa vitabu vipya vya ziada na kiada Chuoni, wakiwemo Book Aid International (UK), Shirika la Misaada la Sweden (Sida) na Elsevier Foundation.

Aidha, Kurugenzi ya Maktaba imefanikiwa kuanzisha *Institutional Repository* (IR) inayowezesha kutunza majarida yote ya machapisho yatokanayo na tafiti mbalimbali zinazofanywa na walimu, wanafunzi na wafanyakazi wengine wa Chuo, zikiwemo *theses na dissertations* zilizofanyika kati ya kipindi cha mwaka

2002 na 2012. Kuanzishwa kwa IR kutasaidia kuongezeka kwa upatikanaji wa haraka wa tafiti za kiafya na kisayansi *(local content)*, zilizofanywa ndani na nje ya nchi na kuondoa gharama za upatikanaji wa tafiti hizi kutoka majarida (*journals*) ya kulipia.

Nachukua nafasi hii vile vile kulishukuru tena Shirika la Misaada la Sweden (*Sida*), Chuo Kikuu cha Dartmouth kupitia mradi wake wa Dar-Dar. Nashukuru sana Taasisi ya Bill and Melinda Gates *(Bill and Melinda Gates Foundation),* kupitia mradi wa ushirikiano kati ya MUHAS na Chuo Kikuu Cha California, San Francisco (*UCSF*) kwa kufanikisha uanzishwaji na uendeshaji wa *multimedia resources* na mafunzo ya matumizi ya kompyuta ndani ya maktaba. Hii ni pamoja na huduma za *Teleconference* na *video conference* ambazo zinaimarisha upatikanaji wa elimu kwa mafunzo ya mbali (*distance learning*) itolewayo kwa kupitia hospitali, taasisi za tiba na vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi.

Aidha, Kurugenzi ya Maktaba imefanikiwa kuanzisha na kuendesha kozi ya "***information and learning technology***" kwa wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza ili kuwajengea uwezo wa utafutaji na utumiaji wa taarifa za kidigitali kupitia mifumo ya TEHAMA.

7. Kurugenzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Utumiaji wa mifumo ya TEHAMA Chuoni umeongezeka sana hivi karibuni kutokana na uhitaji mkubwa wa kuboresha huduma na kuleta tija katika ufundishaji, utafiti na ushauri kwa kutumia teknolojia. Japokuwa majanga yatokanayo na vitu kama moto, mafuriko, n.k. katika mifumo hii ya TEHAMA ni nadra, lakini yanapotokea yanaweza kusababisha madhara makubwa. Kwa kuliona hilo, Chuo kimeanzisha mfumo wa kujikinga na majanga yanayoweza kuathiri mifumo ya TEHAMA (*ICT Offsite Disaster Recovery Site*). Napenda kutoa shukrani kwa Mradi wa Afrique One ulio chini ya uhisani wa shirika la Wellcome Trust la

Uingereza kwa msaada wao mkubwa katika ununuzi wa vifaa vilivyowezesha uanzishwaji wa mfumo huu.

Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na kwa uhisani wa Benki ya Dunia, ipo katika mchakato wa kuunganisha Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti nchini katika mkongo wa TEHAMA wa Taifa. Chuo chetu ni kati ya vyuo 28 vilivyopo katika kundi la kwanza, na kazi ya uletaji na uwekaji vifaa mbalimbali husika katika *Server room* ya Chuo imeanza. Chuo kinapenda kuishukuru sana Serikali kwa uamuzi huo, kwani kukamilika kwa mradi huu kutaleta ahueni kubwa katika gharama za mtandao (Internet) na kwa hivyo kuleta tija na ufanisi zaidi katika utendaji na utimizaji wa maono na malengo ya Chuo.

8. Kurugenzi ya Elimu ya Kujiendeleza na Maendeleo ya Weledi

Katika utekelezaji wa mitaala mipya inayosisitiza umahiri wa mwanafunzi katika kazi anayosomea, Chuo kupitia kurugenzi yake ya Elimu ya Kujiendeleza na Maendeleo ya Weledi imeanzisha mfumo wa kufundisha wa kielektroniki yaani *e-learning platform*. Mpaka sasa wanafunzi 609 na walimu 27 wameshaanza kutumia mfumo huu. Chuo kinaendelea kuwapa mafunzo wanafunzi na walimu wengi zaidi kutumia mfumo huu. Mfumo huu unahakikisha kwamba maelekezo ya mwalimu yanapatikana kwa maandishi na kwa usahihi zaidi kwa kila mwanafunzi na kwa wakati wote. Vile vile mfumo huu unampatia mwanafunzi fursa zaidi ya kufanya majadiliano, mazoezi na mitihani kwa wakati anaokuwa na nafasi na kwa utulivu zaidi. Nachukua nafasi hii kushukuru Chuo Kikuu cha Dartmouth na Skuli ya Afya ya Jamii ya Chuo Kikuu cha Boston kwa kushirikiana nasi katika kufanikisha mradi huu. Pia napenda kukishukuru Kituo cha Kudhibiti Magonjwa cha Marekani (Center for Disease Control and Prevention - CDC) kwa kufadhili mradi huu.

Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa tafiti katika maendeleo ya nchi yetu, Chuo kupitia kurugenzi yake ya Elimu ya Kujiendeleza na Maendeleo ya Weledi kiliendesha kongamano lake la kwanza la kisayansi (*First MUHAS Scientific Conference*) mnamo mwezi Mei mwaka huu. Kauli mbiu ya kongamano hilo ilikuwa ni Tafiti za Afya katika Kupunguza Umaskini (*Health Research Towards Poverty Alleviation*) na jumla ya tafiti 105 zilijadiliwa. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wote. Kipekee kabisa natoa shukrani zetu za dhati kwa Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden (Sida) kwa ufadhili wao mkubwa uliotuwezesha kufanikisha kongamano hili. Chuo kimepanga kufanya kongamano la aina hii kila mwaka, na kwa mwaka ujao kongamano hili limepangwa kufanyika tarehe 14 mpaka 16 mwezi Mei hapa Chuoni. Nachukua nafasi hii kuwaalikeni nyote kushiriki kwenye kongamano hili muhimu litakalojadili kwa kina Tafiti za Afya, Mafunzo na Ubunifu kwa Maendeleo Endelevu (*Health Research, Training and Innovation for Sustainable Development*).

9. Kurugenzi ya Mipango na Maendeleo, Muhimbili

Katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya mwaka 2012/2013, Chuo kiliweza kutekeleza miradi michache ya maendeleo kutokana na ufinyu wa bajeti ya mwaka husika. Miradi iliyotekelezwa iligharamiwa na fedha zilizozalishwa kutoka vyanzo vya ndani na ushirikiano na wahisani. Kwa mfano kwa kutumia fedha kutoka kwa wahisani, Chuo kiliweza kutekeleza miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza ujenzi wa jengo litakalotumika kwa mafunzo ya elimu za afya na elimu ya kujiendeleza (*Center for Health Professions Education*). Ujenzi huu unafadhiliwa na Taasisi ya Bill na Melinda Gates ya Marekani. Mpaka sasa ujenzi huu umefikia asilimia 85% na unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2014. Ujenzi utakapokamilika jumla ya shilingi bilioni 3.8 za kitanzania zitakuwa zimetumika.

(ii) Mwaka 2012/2013 Chuo kiliweza kukarabati maabara za kufundishia zilizopo Muhimbili na Bagamoyo kwa msaada wa Kituo cha Kudhibiti Magonjwa cha Marekani (*Center for Disease Control and Prevention – CDC*). Ukarabati wa maabara za Muhimbili uligharimu shilingi za kitanzania 859,247,738/=. Vile vile shilingi 27,894,037/= zilitumika kukarabati Maabara zilizopo Bagamoyo.

Aidha kutokana na ukosefu wa fedha, Chuo kimeshindwa kutekeleza miradi kadhaa ambayo ni pamoja na ujenzi wa nyumba za wasimamizi wa wanafunzi *(wardens)* wanaoishi mabweni yaliyoko Barabara ya Chole Masaki, ujenzi wa maeneo muhimu ya kupata mahitaji mbalimbali kwa ajili ya wanafunzi kama vile maduka, Internet café na sehemu za kutengeneza nywele (*Students Bazaar*), ujenzi wa sehemu za kufulia nguo wanafunzi, ukarabati wa jengo la Maktaba na ukarabati wa majengo mbalimbali yaliyopo Kampasi ya Muhimbili kama vile, madarasa, maabara na majengo ya utawala.

10. Kurugenzi ya Mipango na Maendeleo, Mloganzila

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, uendelezaji wa kampasi mpya ya Mloganzila unaendelea vizuri. Kwa sasa juhudi zimeelekezwa katika kuweka miundombinu ya maji, barabara na umeme ambayo ni muhimu kwa ujenzi wa hospitali na kampasi mpya. Wakandarasi wa maji, barabara na umeme wameshaanza kazi katika eneo la mradi na maeneo yaliyo nje ya mradi ambayo hayahitaji fidia za mali za wananchi.

Aidha Chuo kimemaliza mchakato na kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya kufundishia na kutoa huduma huko Mloganzila. Majadilialiano yameshafanyika na taratibu za kukabidhi kiwanja zinafuata.

Mchakato huu ulianza upya baada ya kufanya tathmini upya ya gharama za ujenzi kwa sababu gharama za ujenzi zilizokadiriwa mwaka 2009 zilikuwa ni ndogo kulingana na gharama za ujenzi

kwa sasa. Tathmini iliyofanywa na mshauri mwelekezi inaonyesha kuwa kwa sasa gharama ya kujenga hospitali ya vitanda 600 kwa michoro iliyopo ni dola za kimarekani **61,960,000** na fedha zilizopo kwa ajili ya ujenzi ni dola **43,920,000**. Tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia kuongeza kiasi cha dola **18,040,000** ili ujenzi uanze mapema iwezekanavyo. Inatarajiwa ujenzi wa hospitali kuanza mwezi Machi 2014.

Ili hospitali itakayojengwa iweze kutumika kwa kufundishia na kutoa huduma, ni muhimu kukawa na majengo mengine na miundombinu ya kampasi ya Chuo huko Mloganzila, kama vile kumbi za mihadhara, maabara za kufundishia, mabweni ya wanafunzi, jengo la utawala, nyumba za wafanyakazi, na miundombinu mingine muhimu. Chuo kimewasilisha Serikalini makadirio ya ujenzi awamu ya kwanza ambayo inakaribia shilingi bilioni 650. Ni matumaini yetu kwamba Serikali itatusaidia pia katika kufanikisha hili kama ambavyo imekuwa mstari wa mbele katika upatikanaji wa eneo hili, ulipaji wa fidia kwa mali za wakazi waliokuwa katika eneo la mradi na ujenzi wa hospitali ya kufundishia.

11. Taasisi ya Madawa Asili

Chuo kwa kupitia Taasisi yake ya Madawa Asili kimekuwa mstari wa mbele katika tafiti za dawa asili za kutibu magonjwa mbalimbali pamoja na kutoa ushauri ili kuboresha afya za watanzania. Kwa mwaka huu, Chuo kimepata usajili wa Mamlaka ya Chakula na Madawa (TFDA) wa kutengeneza na kusambaza juisi aina ya Morizella ambayo hutumika kama kirutubisho. Usajili huu utaiwezesha Taasisi ya Madawa Asili kuzalisha na kusambaza juisi hii kwa wingi ndani na nje ya mipaka ya Dar es Salaam. Vile vile, Taasisi imeendelea kutafiti na kutengeneza dawa za aina mbalimbali kwa ajili ya matatizo ya pumu, matatizo ya tumbo, matatizo ya uvimbe wa tezi ya uzazi kwa wanaume, matatizo ya ini, matatizo ya magonjwa ya ngozi, na pia

inaendeleza utafiti wa dawa za kupambana na VVU/UKIMWI na malaria.

Pia kwa mwaka huu, Chuo kupitia Taasisi hii kimeanza kutoa mafunzo ya uweledi ili kusaidia uboreshaji wa huduma za tiba zinazotolewa na waganga wa tiba asili. Mafunzo haya yanaelekeza umuhimu wa uweledi katika kutoa huduma kulingana na maadili, miiko na maelekezo ya sera ya Afya ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya mwaka 1990; Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala ya mwaka 2002, pamoja na miongozo inayotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), kanda ya Afrika.

12. Taasisi ya Sayansi Shirikishi za Afya

Kama nilivyoeleza hapo awali, Chuo kupitia Taasisi ya Sayansi Shirikishi za Afya kimeanzisha mafunzo ya jioni katika fani mbalimbali. Uanzishwaji wa mafunzo hayo licha ya kusaidia kuongeza wataalamu wa afya nchini, utasaidia pia kuongeza kipato kwa Taasisi na Chuo, hasa katika kipindi hiki ambacho bajeti ya Serikali haitoshelezi mahitaji halisi.

Aidha, katika harakati zake za kupanua huduma za mafunzo yatolewayo, Taasisi imepanga kuanzisha kozi nyingine fupi na ndefu katika taaluma za afya kuanzia mwaka ujao wa 2014. Taasisi inalenga kupanua huduma hizi za kitiba na kiutafiti wa magonjwa kwenye mikoa mingine nchini.

Vile vile Taasisi ya Sayansi Shirikishi za Afya imedhamiria kufanyia ukarabati majengo yake mbalimbali na kujenga majengo mengine ili kuongeza wigo wa kutoa huduma zake kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla.

12. **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Serikali ya wanafunzi (MUHASSO) ambayo ilisimamishwa mwezi Juni 2011 iliruhusiwa kuanzishwa upya na Baraza la Chuo mnamo mwezi Julai 2013 baada ya wanafunzi kuandika Katiba mpya ya MUHASSO. Harakati za uchaguzi wa uongozi mpya wa

serikali ya wanafunzi zinaendelea. Ni matumaini yangu kuwa serikali mpya itaanza kazi kabla ya mwaka mpya wa 2014.

Aidha ili kuzuia vitendo vya utovu wa nidhamu Chuo kimefanya mapitio ya Sheria ndogondogo zinazosimamia masuala ya wanafunzi *(Students by - Laws)* kwa nia ya kuziboresha. Napenda kukufahamisha kuwa sheria hizo zilikamilika na kupitishwa na Baraza la Chuo mwezi Julai 2013. Vile vile Chuo kimo mbioni kukamilisha sera za huduma za wanafunzi na sera za malazi kwa lengo la kuleta maisha bora na ya utulivu kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Kama alivyosema Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Chuo hiki kimepokea waraka wa Serikali unaoelekeza kikomo cha mikataba ya ajira kwa Wahadhiri, Wahadhiri waandamizi na Maprofesa baada ya kustaafu. Utekelezaji wa waraka huu ni pigo kubwa kwa Chuo kwa kuwa mpaka kufikia mwanzoni wa mwaka ujao, 2014, Chuo kitakuwa kimepoteza wanataaluma wake 19 waliobobea katika fani mbalimbali za afya na wenye uwezo wa kiafya na kiakili, ambao Chuo kinawategemea sana katika ufundishaji, kufanya utafiti na kutoa huduma.

Aidha Chuo kitaendelea kupoteza wanataaluma wake wenye uzoefu na uwezo wa hali ya juu kabisa kwa wingi katika kipindi cha miaka michache ijayo. Ikumbukwe kwamba kwa kipindi cha 1993 hadi 1999 Serikali ilisitisha ajira ya wafanyakazi wa umma hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa wanataaluma. Mpaka sasa pamoja na juhudi nyingi, Chuo hakijafanikiwa kuziba pengo hili. Ni ukweli kuwa wanataaluma wenye uzoefu wa kiwango cha Wahadhiri waandamizi na Maprofesa hasa katika fani za Afya ni adimu sana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi. Japokuwa Chuo kinajitahidi kuajiri wanataaluma katika ngazi za chini, inachukua miaka mingi kuwalea wanataaluma hao na kufikia ngazi hizo. Hivyo basi ili Chuo kiweze kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo, tunaomba Serikali iangalie upya na

kuruhusu kuendelea kuwatumia wanataaluma wastaafu ambao bado wanauwezo wa kutimiza majukumu ya Chuo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Wafanyakazi ni rasilimali muhimu sana katika kutekeleza majukumu ya taasisi kikamilifu. Bila kuwa na wafanyakazi wa kutosha si rahisi kufanikisha malengo ya taasisi na umma kwa ujumla. Hivyo naomba nisisitize kuwa Chuo kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa wanataaluma pamoja na wafanyakazi waendeshaji. Kwa mujibu wa uchambuzi wa mahitaji halisi ya wanataaluma uliofanyika hivi karibuni kwa kutumia vigezo vya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na uwiano wa mwanataaluma na mwanafunzi kulingana na vigezo vya Shirika la Afya Duniani, kwa sasa kuna upungufu wa jumla ya wanataaluma 552 chuoni.

Pamoja na upungufu huu mkubwa bado Chuo kimekuwa na changamoto ya upatikanaji wa vibali vya ajira za kutosha kutekeleza majukumu ya Chuo. Hata vile vibali vichache vinavyopatikana hupatikanana vikiwa vimechelewa sana na hivyo mara nyingine kuwapoteza watu wenye sifa zinazohitajika ambao katika fani za sayansi za afya ni adimu. Napenda kuchukua nafasi hii tena kuiomba Serikali kuidhinisha ajira za wanataaluma mapema kulingana na mahitaji halisi ya Chuo

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Kama alivyotangualia kusema Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Chuo kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa fedha za uendeshaji wa shughuli zake. Fedha zinazoidhinishwa kwa matumizi mengineyo (*Other Charges*) zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka na hivyo kukiweka Chuo mahali pagumu sana kifedha hasa ukizingatia ongezeko la gharama za uendeshaji na kushuka kwa thamani ya shilingi. Aidha kama alivyosema Mwenyekiti wa Baraza la Chuo kwa mwaka huu, Chuo hakikutengewa kabisa fedha ya miradi ya maendeleo (*Capital Development*) kwa ajili ya kampasi ya Muhimbili. Hii ina maana, kwa mwaka huu Chuo

kitapata changamoto kubwa ya kutekeleza mipango yake ya kukarabati kumbi za kufundishia, maabara na mabweni ya wanafunzi ambayo yako katika hali isiyoridhisha kutokana na kukosa ukarabati stahiki kwa muda mrefu. Tunaomba Serikali ituwezeshe kupata fedha za kutosha kukarabati majengo haya.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Majukumu ya Chuo hiki yanagusa moja kwa moja uhai wa binadamu. Hivyo basi, Chuo hakina budi kuhakikisha kwamba huduma zake zote zinatolewa katika kiwango cha ubora wa hali ya juu. Kwa kutambua hilo, Chuo kimeanzisha Kurugenzi itakayoratibu na kusimamia uhakika wa ubora (*quality assurance*) wa huduma zinazotolewa na Chuo. Vile vile Kurugenzi hii itahakikisha kuwa Tafiti na Huduma zote zinakidhi viwango vilivyowekwa, kwa kubuni na kutekeleza mpango mkakati wa uhakiki huu. Ni matumani yetu kwamba katika miaka michache ijayo ubora wa mafunzo, tafiti na huduma zinazotolewa hapa Chuoni utaongezeka kwa kiwango kikubwa na hivyo kuzidi kukiongezea Chuo hiki hadhi ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Kwa kumalizia napenda kuwashauri wahitimu kwamba weledi katika kazi zao wanazoenda kufanya utategemea jinsi watakavyoendelea kujifunza, lakini ni muhimu sana kwao kuzingatia kanuni na miiko ya mabaraza ya fani zao, na kuzitekeleza ipasavyo. Napenda pia kuwatakia maisha mema yenye mafanikio huko muendako. Kama ilivyo kawaida tunategemea mtaendelea kuwa mabalozi wazuri wa Chuo hiki, popote pale mtakapopangiwa kazi.

Mwisho kabisa naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Maprofesa, Maprofesa Washiriki, Wahadhiri Waandamizi, Wahadhiri, Wahadhari wasaidizi na Wafanyakazi wengine wote wa Chuo hiki kwa kushiriki kikamilifu na kuhakikisha kwamba wanafunzi hawa wanaohitimu na wengine wote wa Chuo hiki

wanapata elimu itakayowawezesha kutekeleza majukumu yao huko waendako.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, wageni waalikwa, mabibi na mabwana,

Asanteni kwa kunisikiliza na nawatakieni maadhimisho mema ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2014.

MWISHO

14 Desemba, 2013